**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 18 Juni, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Sita, Bilioni Mia Tisa Themanini na Mbili, Milioni Sabiini na Sita, Tisiini na Nane Elfu na Elfu Thelathini na Saba Kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Siku ya Tarehe Thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Sita, Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

194. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Tathmini ya matumizi ya mifuko mbadala iko vipi kwa sasa baada ya katazo la mifuko ya plastiki kutokana na madhara yake makubwa kwa jamii.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

96. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kiasi gani taasisi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) inatimiza malengo ya kuwakomboa wananchi kupitia mikopo na mafunzo wanayoyatoa.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

258. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa za hivi karibuni zinaonesha mwenendo mzuri wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kutokana na usimamizi mzuri na uwekezaji uliofanywa.

Je, kuna ongezeko la kiasi gani la faida ya PBZ inayotokana na mali (Return on Asset) na ile inayotokana na mtaji (Return on Equity) kwa kipindi cha 2022 - 2024.

### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

125. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Sera ya ardhi ina mtazamo gani chanya katika kuendeleza utaratibu wa kupunguza na hatimae kuondosha kabisa migogoro ya ardhi hapa nchini.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

273. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tathmini ya Tume ya Utangazaji ikoje katika suala zima la udhibiti wa maadili ya vyombo mbali mbali vya habari nchini.

**Wizara ya Afya:**

304. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya kazi nzuri ya kuimarisha miundombinu ya afya kwa kujenga hospitali za kisasa. Hata hivyo, baadhi ya hospitali hizo kama vile hospitali ya Lumumba, wapo wataalamu wazuri lakini kuna uhaba wa baadhi ya vifaa muhimu vya tiba kama vile vya kutibu magonjwa ya mfumo wa mkojo ambayo yameongezeka hivi sasa.

Je, Serikali imezingatia vipi umuhimu wa kupatikana vifaa muhimu hivyo ili kuwaondolea usumbufu wagonjwa wetu ambao wengine wanasafiri kwenda Tanzania bara kufuata huduma hizo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

30. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na malalamiko juu ya utozaji mara mbili wa tozo ya kusafirisha magari baina ya bandari ya Unguja na ile ya Mkoani Pemba. Tozo hizi zinaleta mkanganyiko mkubwa kwa wananchi wanaotaka kusafirisha magari yao kwenda Pemba kipindi cha likizo na mwisho wa mwaka.

(a) Pamoja na kuwa tatizo hili ni la muda mrefu, je kwa kiwango gani Serikali inalitambua tatizio hili.

(b) Je, kufanya hivi si kuua kauli mbiu ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya kuifungua Pemba kimaendeleo.

(c) Je, ni gharama gani hasa mtu hutakiwa kulipa anaposafirisha gari baina ya Unguja na Pemba.

187. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Bado suala la uvamizi wa maeneo tengefu ya barabara linaonekana kusuasua.

(a) Ni nani anawajibika na jukumu hili.

(b) Je, Wizara haioni kwamba kulichelea jambo hili kunaipa Serikali gharama za fidia kubwa wakati wa utanuzi wa barabara.

281. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Je, Serikali imezifanyia kazi vipi changamoto zilizoibuka katika zoezi la ulipwaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

189. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:
Tathmini iko vipi juu ya kilimo cha zao la kungu manga Zanzibar.

222. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Uwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kiasi gani mabadiliko ya tabianchi yanaathiri uzalishaji wa maziwa kwa wajasiriamali wadogo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

249. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kupitia mapato yanayotokana na uvuvi wa bahari kuu kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

290. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa muda mrefu Zanzibar imetegemea utalii wa maumbile ya kiasili na utamaduni ambao katika nchi zilizoendelea umeanza kupungua kasi.

Vipi Wizara yako imejidhatiti na kuanzisha aina mpya za utalii kama vile utalii wa ndani wenye kuratibiwa vyema, utalii wa kimatibabu, utalii wa matamasha na matukio, utalii wa michezo, utalii wa meli (Cruz ship) na utalii wa teknolojia mnemba (Artificial intelligence tourism).

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Sita, Bilioni Mia Tisa Themanini na Mbili, Milioni Sabiini na Sita, Tisiini na Nane Elfu na Elfu Thelathini na Saba Kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Siku ya Tarehe Thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Sita, Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Pili.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Pili.

Zanzibar,
18 Juni, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR.